

## Wizara ya Mifugo na Uvuvi yafunguka

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema haijawahi kuzuia uvuvi wa kamba koche licha ya kufanyika marekebisho ya sheria ya uvuvi.

Hayo yalisemwa bungeni jana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega wakati akijibu swali la Mbunge wa Kibiti, Twaha Mpembenwe (CCM).

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji, ni lini serikali itatoa uamuzi wa kuwaruhusu wavuvi wa kamba koche kuvua kuanzia mwezi Desemba hadi Julai kila Mwaka?

Akijibu swali hilo, Ulega alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi namba 22 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020, serikali haijawahi kuzuia uvuvi wa Kamba Koche.

Alifafanua kuwa Serikali imeweka utaratibu kwa ajili ya uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo na wakubwa.

Alieleza uvuvi wa

Kambamiti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo unaruhusiwa kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Septemba kila mwaka kwa ukanda wa Kaskazini unaohusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Chalinze na kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti kila mwaka kwa ukanda wa Kusini unaohusisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Kilwa.

Aidha, alifafanua kuwa kipindi kilichobaki kimeachwa ili Kambamiti wazaliane na kukua.

Alisema maamuzi haya yamefanyika baada ya taarifa za utafiti wa Kisayansi na kuzingatia uendelevu wa rasilimali hii.

"Serikali imekuwa ikisisitiza kwa wadau wote wa uvuvi hususani uvuvi wa Kambamiti kufanya shughuli zao kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu kwa maslahi mapana ya vizazi vilivyopo na vijavyo," alisisitiza.

## Wachangia maji na mifugo

**Handeni.** Wananchi wa kijiji cha Gendagenda mkoani Tanga wamemwambia Mkurugenzi mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), Clement Kivegalo na mbunge wa jimbo hilo, John Sallu kuwachimbia mabwawa ya maji ya kunywa, kwani kwa sasa wanachangia na mifugo. "Nitatuma timu kwa ajili ya kuangalia sehemu ya kuchimba visima kwa ajili ya huduma za muda mfupi na mrefu," alisema Kivegalo.

**(Rajabu Athumani)**



## HABARI BUNGENI

### 'Serikali haijazuia uvuvi wa kamba koche'

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa haijawahi kuzuia uvuvi wa kamba koche.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibiti (CCM), Twaha Mpembenwe.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itatoa uamuzi wa kuwaruhusu wavuvi wa kamba koche kuvua kuanzia mwezi Desemba hadi Julai kila mwaka.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 na marekebisha yake ya mwaka 2020, serikali haijawahi kuzuia uvuvi wa kamba koche.

Hata hivyo, alisema serikali imeweka utaratibu kwa ajili ya uvuvi wa kambamiti kwa wavuvi wadogo na wakubwa.

"Uvuvi wa kambamiti kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo unaruhusiwa kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Septemba kila mwaka kwa ukanda wa kaskazini unaohusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Chalinze na kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti kila mwaka kwa ukanda wa kusini unaohusisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Kilwa," alisema.

Ulega alisema kipindi kilichobaki kimeachwa ili Kambamiti wazaliane na kukua.

"Uamuzi huu umefanyika baada ya taarifa za utafiti wa kisayansi na kuzingatia uendeleu wa rasilimali hii," alisema.

Ulega alisema serikali imekuwa ikisisitiza kwa wadau wote wa uvuvi hususani uvuvi wa kambamiti kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu kwa maslahi mapana ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

## Seri

# W

imepatiwa ioni 80 n kununua uhaba uli vya kutole msingi.

Naibu V Tawala za Mitaa (TA Dugange, bungeni, swali la M um (CHA



Baadhi y Gofrey f HIM JOS